# U-Nigeria: Athari zake katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania

G.A. Kasiga

**Ikisiri**

Makala haya yanaangazia athari za U-Nigeria katika filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Dhana hii ya U-Nigeria imetazamwa kama masuala yanayojadiliwa katika filamu za ki-Nigeria ambayo yamekuwa yakipatiwa nafasi ya kujadiliwa upya katika filamu za Kitanzania. Kupitia makala haya, filamu ya Kiswahili nchini Tanzania imeonekana inahitajika kuwa alama ya utambulisho wa utamaduni wa Kitanzania. Athari za U-Nigeria zimejadiliwa katika pande mbili: Athari za U-Nigeria kwa watayarishaji wa filamu za Kiswahili - Tanzania na athari za U-Nigeria kwa watazamaji wa filamu za Kiswahili -Tanzania. Tija na madhara ya U-Nigeria yamejadiliwa katika muktadha wa utayarishaji na utazamaji. Kwa kuhitimisha hili, imeonekana kuwa jamii inayoazima utamaduni wa jamii nyingine katika utambaji wa hadithi zake huiweka mbali sanaa na jamii husika. Hivyo, watayarishaji wa filamu za Kiswahili-Tanzania wanahitajika kutayarisha filamu ambazo zitakuwa sehemu ya tajiriba, silika, historia na maisha ya Kitanzania.

## 1.0 Utangulizi

Kabla hatujaingia ndani kutazama athari za U-Nigeria katika filamu za Kiswahili-Tanzania ni vizuri tukiifafanua dhana hii ya U-Nigeria ambayo ni msingi mkuu wa makala haya. Dhana hii ya U-Nigeria katika hoja yoyote itakayojengwa katika makala haya yatamaanisha hali na masuala yatokanayo na jamii ya wa-Nigeria yaliyomo kwenye filamu zao, ambayo huibuka katika filamu za Kiswahili zinazotayarishwa nchini Tanzania. Tumeuangalia U-Nigeria katika maeneo kadhaa yaliyohusisha eneo la utambaji wa hadithi linalogusa uandishi, uongozaji, uchukuaji picha jongefu, uigizaji, maleba, mapambo, upangaji wa vionwa, maudhui makuu ya filamu, uhariri wa matukio ya hadithi ya filamu pamoja na njia zinazotumika katika usambazaji wa filamu kwa hadhira ya Kitanzania.

Kwa kiasi kikubwa, makala haya yanasukumwa na Nadharia ya Upembetatu wa Ki-Aristotle inayoiona sanaa kama zao la kijamii. Hivyo, iwapo sanaa ni zao la jamii, basi kwa kiasi kikubwa filamu zinazotayarishwa nchini Tanzania, zinapaswa kuwa alama ya Utanzania uliozaa filamu hizo

(Kasiga, 2013). Tunaamini kuwa Utanzania huo huzungukwa na mambo mengi ya kimsingi yanayojenga jamii husika ambayo kwayo lugha huwa kiungo chake muhimu. Masimbi (2010) kupitia makala yenye kichwa cha habari cha "Kifo cha Utamaduni wa Mtanzania" yanayochambua namna utu na maendeleo unavyotegemea misingi imara ya utamaduni na sanaa katika ufanikiwaji wake, anasema:

> Katika duru nyingi za kimataifa, nchi yetu ilipata kusifiwa kwa jitihada zake za kushughulikia ukuzaji wa utamaduni. Hata hivyo, kwa hali ilivyo sasa na kama hatua za dhati hazitachukuliwa, kazi iliyofanywa miaka ya nyuma, hasa mara baada ya uhuru na miaka takribani 20 iliyofuata, itapotea na tutajikuta tukiwa taifa lisilo na utamaduni wake. Siyo hilo tu, tutajikuta pia tukiwa taifa lenye raia wasio na mwelekeo, wasiojifahamu, wasio na fahari ya utaifa wao, wasio na umoja, mshikamano au heshima mbele ya mataifa mengine.

Kwa hakika, hakuna asiyekubali kuwa utamaduni huipa jamii utambulisho; pia huitofautisha jamii moja na nyingine. Zaidi, huweza kuonesha mambo mazuri na mabaya katika jamii husika kuendana na miktadha ya jamii husika. Si hivyo tu, pia huweza kutoa suluhisho la masaibu mbalimbali ya kijamii kulingana na miktadha ya kiutamaduni iliyochorwa kupitia jamii husika. Ni dhahiri kabisa kuwa sura na haiba ya jamii huweza kueleweka na kuelezeka kirahisi kupitia utamaduni wa watu wake. Utamaduni huweza kuhamishwa kutoka kizazi hadi kizazi kupitia lugha, sanaa na imani za kiroho. Aidha, mila na desturi wanazofuata, matamasha au sherehe wanazoendesha, mavazi yao, chakula chao na taratibu nyingine za utamaduni wanazofuata huunganisha jamii.

Inaaminika kuwa utamaduni ndio "kidhibiti mwendo" kinachoongoza mwenendo wa tabia za watu katika jamii. Vilevile, ndio msingi wa maisha ya mtu binafsi kumwezesha kujitambua, kuwa na mwelekeo na kujichagulia falsafa sahihi ya maisha yake. Pia, utamaduni ni msingi wa maendeleo na ubunifu katika jamii. Katika dunia hakuna jamii inayokua kwa kurudufu utamaduni wa jamii nyingine. Inachoweza kufanya ni kuchota baadhi ya maarifa inayoyaona ni muhimu kwa mustakabali wa jamii yake. Kuchota huko hufanywa kwa kuongeza ubunifu kwa maarifa yaliyochotwa na kuyasogeza mbele zaidi kufuatana na idili za jamii iliyochukua ufundi huo wa jamii nyingine.

Kwa hiyo, ni bayana kuwa ili kuweza kujenga filamu iliyo madhubuti kama sanaa nyingine za kifasihi, hatuna budi kuwa na sanaa iliyojengwa kutoka katika misingi ya jamii na utamaduni inayoakisi maisha ya wanajamii husika. Katika kushadidia hili, Madumulla (1993: 143-144), anasema:

> …kauli ya kisanaa inasemekana kuwa ni kweli ikiwa imeakisi vizuri uhusiano wa mtu na ukweli wa asili na wa kijamii. Uakisi sahihi hupata msingi wake katika jumuiko la mambo mawili: ufahamu wa kisanaa wa ukweli, na ubora wa kiujumi wa ukweli. Katika maelezo ya kisanaa, msanii hujihusisha zaidi na jinsi ambavyo jambo lingewezekana kutokea au jinsi ambavyo lingefaa litokee lakini katika hali halisi halikutokea au halijatokea hivyo.

Hivyo, ni sawa na kusema kuwa nguvu ya usanii hutokana na uzoefu wa msanii katika mazingira yake na kiwango cha ufahamu wake. Umuhimu wa kazi ya sanaa kwa jamii unatokana na jinsi msanii anavyohusisha usanifu wake na matukio muhimu yanayomzunguka. Hakuna shaka kwamba kuna mapatano makubwa kati ya msanii, kazi ya sanaa na hadhira yake. Mapatano haya ya kijamii licha ya kuisogeza sanaa mahali pake stahiki, yaani kwa wanajamii wake, pia huleta ukamilifu wa mawasiliano baina ya sanaa na wanajamii wake.

Fauka ya hayo, katika kuzidi kuhusianisha yanayowasilishwa na filamu, hali ya maisha ya mtu au jamii inayolengwa na kazi ya filamu, Nichols (1991:xiii), anasema:

> *What films have to say about the enduring human condition or about the pressing issues of the day can never be separated from how we say it.*
>
> Filamu zinapojadili masuala yanayomkumba mwanadamu au mambo yanayomkwaza kila siku hazitakiwi kwenda mbali na jinsi yalivyo (tunavyoyaona na kuyasema) (Tafsiri yetu).

Kutokwenda mbali huko ambako tunaamini Nichols anakuzungumzia bado kunazidi kurejelea mahusiano ya upiramidi ama upembetatu baina ya msanii, kazi ya kisanaa na jamii. Hii ni sawa na kusema kuwa mawasiliano yaliyokamilika ya kazi ya kisanaa kutoka kwa msanii aliyejenga kazi hiyo kwenda hadhira yake yanapaswa kwenda sambamba na mazingira na jadi za jamii husika (utamaduni). Namna mambo yalivyo katika jamii, yanahitajika kusemwa bila ya kwenda mbali na yanavyoonekana huku yakitiwa nakshi na ufundi wa kisanaa ili yasiwachoshe wapokeaji wake.

Ruhumbika (1983, 2003: 262) naye katika kuzidi kuupigia "mkoko" usuhuba wa lugha, fasihi na utamaduni katika mawasiliano ya mwanadamu, anaona ukuzaji wa fasihi ya Kiswahili ulivyo na umuhimu mkubwa katika jitihada za kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Akirejelea namna fasihi ilivyo sehemu muhimu sana katika utamaduni wa binadamu, anasema:

> Lugha ndiyo chombo kikuu cha kwanza na kikuu kuliko vyote cha mawasiliano kati ya binadamu na binadamu mwenzake katika jamii; kwa hiyo ndicho chombo muhimu kuliko vyote

> katika uundaji wa jamii, ikiwa ni pamoja na utamaduni wake katika vipengele vyake vyote. Ni wazi kwamba, fasihi ambayo ni sanaa inayotumia lugha, kwa uumbaji wake, ni sehemu yenye maana kubwa sana katika utamaduni wa jamii yoyote ile, wala si nyongeza tu kwenye utamaduni wake.

Filamu, kama fasihi iliyoibuka kwenye dhana ya usimulizi bunilizi kwa kutumia nyenzo za kiteknolojia, nayo ni sanaa ya lugha itumiayo mbinu za kitazamaji katika kuyaona matendo yanayoigizwa na wahusika katika runinga. Filamu ni nuru thabiti ya kuuona ukweli wa jamii na kuzama ndani ya ukweli huo ili kuiwezesha jamii kuuelewa vyema. Aidha, kama ilivyo kwa fasihi, filamu ni nyenzo muhimu kabisa kwa maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na hali ya binadamu (Marx & Engles, 1976). Ni dhahiri kwamba fasihi (filamu ikiwamo), ni sanaa thabiti katika kumfikisha mwanadamu kwenye kiini cha ukweli wa jamii yake na kuiwezesha jamii hiyo kupata mantiki yake na kisha kuipa nguvu ya kupiga hatua katika kujiletea maendeleo. Hivyo, filamu za Kiswahili nchini Tanzania zinatarajiwa kuwa kiini cha ukweli wa kijamii ili kuipa uhai jamii hiyo na si kwenda kinyume na mapatano yasiyoweza kutenganishika kati ya msanii, kazi ya sanaa na hadhira. Kwa hali ilivyo ni hakika kuwa U-Nigeria umeleta athari kwa filamu za Kiswahili nchini Tanzania. U-Nigeria uliojipenyeza katika filamu za Kiswahili nchini Tanzania umekuwa ukiyatenganisha mapatano yanayopaswa kuwapo baina ya filamu za Kiswahili na jamii ya Kitanzania.

## 2.0 Athari za U-Nigeria kwa Watanzania

Kama tulivyojaribu kujenga picha hapo awali kuhusu sanaa, utamaduni na jamii, tutaona kuwa filamu, kama zilivyo sanaa nyinginezo, haijifungi kwenye ombwe tu. Filamu huwa si sanaa ya mtu fulani tu, bali huwa ni sanaa yenye kuakisi maisha ya mtu huyo kulingana na wakati fulani pamoja na mazingira fulani yenye kutoa majawabu ya matatizo yanayomghasi. Masuala hayo huwa ni yale yanayoizuguka jamii anayoishi. Kwa hivyo, jamii na sanaa huwa katika mapatano ambayo hayawezi kugawanyika au kutenganishwa. Mapatano hayo yanayooneshwa katika filamu kwa namna kubwa huwa na uhalisi na masuala ya kijamii yaliyopo katika jamii ijapokuwa masuala hayo huboreshwa kwa kuongezewa vionjo vya kibunifu ili yaweze kuwasilishwa vyema na kuleta athari iliyokusudiwa kwa jamii itakayopokea sanaa hiyo.

Athari za U-Nigeria kwa jamii ya Kitanzania tumeziweka katika makundi mawili. Kundi la kwanza limehusisha athari za U-Nigeria kwa watayarishaji wa filamu za Kitanzania. Athari hizi zimechanganuliwa kwa uhasi na uchanya wake kwenye utayarishaji wa filamu za Kitanzania. Kundi la pili limechanganua athari za U-Nigeria kwa watazamaji wa filamu za Kitanzania.

Vivyo hivyo, athari za U-Nigeria kwa watazamaji wa filamu za Kitanzania nazo zimetazamwa kwa uhasi na uchanya wake, yaani madhara na tija zake.

### 2.1 Madhara ya U-Nigeria kwa Watayarishaji wa Filamu za Kiswahili nchini Tanzania

Hali ya filamu za ki-Nigeria kuwa kivutio kwenye utayarishaji wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania imeufanya U-Nigeria kuwa motifu na kionjo muhimu cha utayarishaji wa filamu za Kiswahili. Hii imesababisha filamu za Kiswahili kuwa mbali na uhalisi wa maisha pamoja na uhalisia wa masuala ya kimaisha ya jamii ya Kitanzania yanayojadiliwa kwenye filamu hizo. Watayarishaji wa filamu za Kitanzania wamesababisha filamu wanazozi-tayarisha kukosa ukweli wa uhalisi, yaani ukweli wa matukio, dhamira, ujumbe na falsafa zinazopatikana kupitia filamu wanazozitayarisha.

Ukweli wa kisanaa nao umekuwa mgumu kupatikana kutoka katika filamu wanazozitayarisha. Mwigo wa utayarishaji wa filamu za ki-Nigeria umeleta mfanano katika utayarishaji wa filamu katika jamii hizi mbili (Kitanzania na ki-Nigeria). Kufanana huko kumeacha athari kwa watayarishaji wa filamu za Kitanzania ambao kwao ubunifu umekuwa ukitegemea maendeleo ya ubunilizi wa ki-Nigeria. Utegemezi huo umewaacha watayarishaji wa filamu za Kitanzania kuonekana ni "warudufu" wa utayarishaji wa filamu wa ki-Nigeria (Kasiga, 2013). Katika kushadidia hili, Mfwaisa[1] (2013) anasema:

> Athari zitokanazo na U-Nigeria ni kukosa ubunifu, filamu zetu kushindwa kupenyeza soko la kimataifa lakini baya zaidi ni kupoteza utamaduni wetu na kukosa alama ya Utanzania; jambo hili limefanya tasnia ya filamu kudumaa na kushindwa kabisa kukua japo kuna watu wanaofikiri imekua kwa kuwa na utitiri wa filamu sokoni huku wasanii wakiwa wapo palepale kisanaa bila kupiga hatua, hakuna msanii anayejua chochote kuhusu taaluma ya filamu, jambo ambalo ni mbaya tunapoelekea kwenye shirikisho la Afrika mashariki, kila kitu tunaweza kuiga lakini tunaishia katika kuiga bila kuendelea.

Katika kuendelea kudodosa kuhusu athari za U-Nigeria kupitia majadiliano ya makundi yanayojumuisha watayarishaji wa filamu za Kitanzania ilionekana U-Nigeria umeleta madhara katika kukua kiubunifu kwa watayarishaji wa filamu za Kitanzania. Kupitia maoni ya mtayarishaji wa filamu za Kitanzania, Bw. Apilike Gordon, akirejelea mwigo wa utayarishaji wa filamu za Kitanzania unaoleta athari hasi za ubunifu kwa watayarishaji wa filamu za Kitanzania, anasema:

---

[1]Myovela Mfwaisa ni mwandishi wa makala za filamu na wasanii magazetini, mtayarishaji wa filamu za Kitanzania, na mmiliki mwenza wa http://filamucental.co.tz. Mahojiano yamefanyika kupitia mtandao wa facebook Aprili 29, 2013.

> Mkuu John Kallapics tatizo tumewachukua wa-Nigeria kuwa ndio *role models* (watu wetu wa kuwaiga) kwenye filamu, unategemea nini hapo? *Film industry* (tasnia ya filamu) ya Afrika ni pana sana na haiishii Nigeria peke yake... Hebu niulize swali... ni wangapi wanamfahamu Sembene Ousmane-Mkongwe wa filamu za ki-Afrika? Wangapi wamewahi kuona kazi zake?[2]

Maoni ya Bw. Gordon yalikuwa yakishadidia kuhusu athari hasi ambayo watayarishaji wa filamu za Kitanzania wameipata kutoka katika utazamaji wao wa filamu za ki-Nigeria. Mwigo wa utayarishaji wa filamu za Kitanzania umezifanya filamu hizo kuwa sehemu ya pili ya utayarishaji wa filamu wa ki-Nigeria. Apilike anaona kuwa kuna haja ya watayarishaji wa filamu za Kitanzania kutojifunga katika kuitazama *Nollywood*[3] pekee katika kuchukua mbinu za utayarishaji wa filamu. Utayarishaji bora wa filamu ni ule unaotazama filamu kutoka mataifa mbalimbali na kuchota amali zitakazowawezesha kutamba hadithi zinazowaelezea.

Madhara haya ya uchotwaji wa U-Nigeria na kuwekwa katika filamu za Kiswahili nchini Tanzania kiubunifu yamesababisha filamu za Kiswahili kutokuwa na mshikamano wa matukio ya kihadithi na utambaji wake. Matukio hayo kwa mfano katika filamu za *Nsyuka* (2003) na *Odama* (2007) yamekuwa yakionekana bayana, Mathalani, katika filamu ya *Nsyuka* (2003) iliyoongozwa na Mussa Banzi utaona uwapo wa kipande cha igizo kinachoanzisha filamu kukosa mapatano na hadithi kuu inayotambwa. Kukosekana huko kwa mapatano kati ya matukio hayo yaliyopo ndani ya filamu kumeonekana kuwa ni mwigo uliotoka kwenye filamu za kutisha za ki-Nigeria ambazo huweka vipande vingi vya utangulizi vya mchezo visivyo kuwa na mwendelezo wa hadithi ya filamu inayotambwa.

Katika filamu hiyo, kipande kinachoanzisha filamu kinamwonesha Doreen akishuka ndani ya gari kisha akifungua geti na kuingia ndani. Humo anakutana na mzoga wa mbwa uliotapakaa damu na maiti zenye majeraha ya kutisha. Maiti hizo ni za jamaa aliokuwa akiishi nao. Akiwa ndani ya nyumba, anatokewa na *Nsyuka* (mzimu). Kipande hicho cha mchezo kinapoisha ndipo filamu inaanza. Sasa, kipande hicho cha mchezo kikihusishwa na ploti ya hadithi inayotambwa vinakuwa ni visa viwili visivyoumana.

Vilevile, kimuundo urefushwaji wa matukio ya namna hiyo huwa na lengo la kuifanya filamu iwe na sehemu ya kwanza, ya pili, ya tatu na kuendelea kama inavyoonekana katika filamu ya *My Dreams* (2010), *Devil Kingdom* (2011), *Odama* (2007) na *Young Bilionaire* (2010). Kwa mfano,

---

[2] Maoni haya yamechukuliwa tarehe 28-1-2013 kutoka http://facebook.com/Taff tuongee

[3] Lakabu inayorejelea tasnia ya utayarishaji wa filamu za ki-Nigeria..

kupokewa vyema sokoni kwa filamu ya *Nsyuka* (2003) kulifanya zifuatie *Nsyuka II* na *Nsyuka III.* Muundo huu umerithiwa kutoka katika utayarishaji wa filamu za ki-Nigeria. Jambo hili limekuwa likienda sambamba na utumiaji wa majina ya filamu kwa lugha ya Kiingereza huku filamu zikiwa zimendikwa kwa lugha ya Kiswahili. Maleba na mavazi nayo yamekuwa yakiufuata U-Nigeria kwa kuiga mavazi ya kijadi ya Ki-Yoruba, Ki-Igbo na Ki-Hausa yanayochukua nafasi katika utambaji wa filamu za ki-Nigeria (Kasiga, 2013).

Fauka ya hayo, kuna wakati kuliibuka filamu zinazoishia na maneno ya Kiingereza ya *In God we trust* (Mola ndiye tumwaminiye) kila mwishoni mwa filamu ya Kitanzania. Uwekaji wa maneno hayo ulitokana na kuiga filamu za ki-Nigeria zilizokuwa zimebeba maudhui ya Ukristo (ulokole). Filamu nyingi za ki-Nigeria zilikuwa na maneno hayo pindi tu filamu husika inapokwisha. Mtindo huu pia ukawa unaonekana katika filamu zilizokuwa zikitayarishwa na kampuni ya Game 1$^{st}$ Quality ya Tanzania kama kionjo katika uwasilishaji wa filamu za Kiswahili (Kasiga, 2013).

## 2.2 Tija za U-Nigeria kwa Watayarishaji wa Filamu za Kitanzania

Tukiachana na madhara yanayoonekana kuletwa na U-Nigeria katika filamu za Kitanzania, mwigo wa utayarishaji wa filamu za ki-Nigeria umeweza kuleta soko la utayarishaji wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania ambao hapo kabla haukuwapo. Katika mapambano ya kuleta sanaa ya filamu itakayokuwa na mashabiki wengi, watayarishaji wa filamu za Kitanzania waliamua kutayarisha filamu zenye kufuata motifu, ishara na mtindo wa ki-Nigeria katika kutayarisha filamu zao. Mtindo, motifu za ki-Nigeria, maudhui yaliyozoeleka kuonekana katika filamu za ki-Nigeria, pamoja na mfumo wake wa usambazaji na uuzaji ndio vimeleta sanaa maarufu ya filamu za Kitanzania zinazozidi kuchukua kasi kila uchwao.

Mbinu za awali za watayarishaji wengi wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania zilipatikana kutoka filamu za ki-Nigeria. Watayarishaji waliweza kujifunza mbinu za utayarishaji wa filamu kupitia filamu mbalimbali za ki-Nigeria walizokuwa wakizitazama kama sehemu yao ya kupata ujuzi wa utayarishaji wa filamu. Uangaliaji huo wa filamu za ki-Nigeria uliwapa mbinu za uchukuaji picha jongefu kwa kamera za video za kidijitali, kutumia programu mahususi za uhariri wa picha jongefu, uongozaji wa filamu pamoja na mbinu kadhaa za usambazaji na uuzaji wa filamu. Mambo hayo waliyojifunza kutoka kwenye filamu za ki-Nigeria yaliwapa ari ya kutayarisha filamu zao. Ari hiyo imezifanya filamu wanazozitayarisha kushika soko la ndani la filamu pamoja na kuenea katika nchi nyingine za jirani zinazozungumza lugha ya Kiswahili.

Muungano baina ya waigizaji na watayarishaji filamu wa Kitanzania na wa ki-Nigeria nao umekuwa sehemu ya mafanikio ya utayarishaji wa filamu za

Kitanzania. Kwa hivi sasa, utayarishaji wa filamu za Kitanzania umekuwa na ushirikiano na watayarishaji na waigizaji wa ki-Nigeria kiasi cha kutayarisha filamu zinazowahusisha wasanii kutoka nchi hizo. Ushirikiano huo umeweza kuzaa filamu za *Dar To Lagos* (2006), *Penina-The Jezebel's Daughter* (2006), *She Is My Sister* (2006), *Unfortunate Love* (2009), *The Director* (2006), *Devil Kingdom* (2011) na *Day After Death* (inatayarishwa). Pia, umekuza uhusiano baina ya wa-Nigeria na Watanzania. Wasanii maarufu wa ki-Nigeria kama vile Bimbo Akintola, Mercy Johnson, Mzee Emanuel France, Nancy Okeke, Ramsey Nouh, Van Vicker na Femi Ogedegbe wameweza kushirikiana na wasanii maarufu wa Kitanzania kama vile marehemu Steven Kanumba, Yvonne Cherry, Kajala Masanja, Lisa Jensen, Mahsen Awadh, Emanuel Myamba, Adam Melele, Abdul Ahmed na Hashim Kambi. Mahusiano hayo ya kikazi yamesaidia filamu za Kitanzania kuongeza ukubwa wa soko lake kuendana na mipaka ambayo filamu za ki-Nigeria hufika. Vilevile, mtayarishaji na msambazaji wa filamu za Kitanzania, Mtitu Game 1st Quality, ameweza kuingizwa/kusajiliwa kwenye kundi la watayarishaji wa filamu nchini Nigeria kutokana na filamu alizozitayarisha kwa kuwashirikisha wasanii wa ki-Nigeria.

Filamu za Kitanzania, licha ya kuwa na U-Nigeria, zimeweza kutoa ajira kwa vijana waliojiingiza katika utayarishaji wake. Watanzania wameweza kuajiriwa kwenye soko la utayarishaji wa filamu kama waandishi wa miswada, waigizaji, wabunifu wa maleba, wapambaji wa waigizaji, waongozaji filamu, wahariri, wasambazaji, wauzaji wa kawaida, waonesha filamu za video kwenye *vimkandala*[4] pamoja na maeneo mengi mengine ya ajira yanayohusisha uzalishaji wa filamu.

Bajeti ndogo zinazotumika katika utayarishaji wa filamu hizi ambazo ni mwigo kutoka utayarishaji wa filamu za ki-Nigeria, zimewawezesha watayarishaji kutayarisha filamu za kuwaingizia kipato. Mwanzoni, utayarishaji wa filamu ulikuwa ukitegemea misaada kutoka serikalini ama kutoka katika taasisi za kigeni. Filamu zilizokuwa zikitayarishwa kupitia misaada hiyo ya fedha zilikuwa zikisawiri malengo na sera za taasisi hizo. Matokeo yake ni filamu zilizokuwa zikisawiri masuala ya UKIMWI, umaskini, ukandamizwaji wa wanawake au masuala kuhusu watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu. Mara nyingi, mahitimisho yaliyokuwa yakitoka katika filamu hizo hayakuwa yakiakisi jamii ya Kitanzania zaidi bali yaliakisi malengo ya taasisi hizo. Filamu hizo wakati mwingine zilisahau dhima ya kuburudisha na kuegemea katika kutoa elimu tu.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye filamu za Kitanzania zenye athari ya U-Nigeria yamesaidia kuieneza lugha hii adhimu katika ukanda wa

---

[4]Hivi ni vibanda vidogo vya kuoneshea filamu vinavyopatikana katika mitaa wanayoishi watu wa hali ya chini nchini Tanzania

Maziwa Makuu na maeneo mengine ya Afrika na hivyo kutoa mchango katika uenezaji wa lugha ya Kiswahili. Karibu filamu zote za Kitanzania hutumia lugha ya Kiswahili. Filamu za Kitanzania zilizotayarishwa kwa kuwatumia waigizaji wa ki-Nigeria, sehemu ya dayolojia zake hutumia lugha ya Kiingereza ingawa bado sehemu kubwa ya filamu ikitumia lugha ya Kiswahili. Matumizi haya ya lugha ya Kiswahili huku kukiwa na tafsiri ya maneno kwenda kwenye lugha ya Kiingereza, yamechangia katika kuieneza lugha ya Kiswahili. Umaarufu wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania pia umechangia kuanzishwa kwa stesheni ya *African Magic-Swahili* na *Maisha Magic Bongo* ikiwa ni sehemu ya kituo cha runinga cha kulipia cha *DSTV*. Stesheni za *African Magic-Swahili* na *Maisha Magic Bongo* hurusha filamu na drama za runinga za Kiswahili kwa saa ishirini na nne. Ukitazama vizuri utaona kuwa kupitia filamu za Kiswahili nchini Tanzania lugha ya Kiswahili imekuwa bidhaa muhimu ya kuwezesha ubunifu wa filamu hizi kufanyika na kuwezesha watayarishaji kujipatia kipato.

## 3.0 Madhara ya U-Nigeria kwa Watazamaji wa Filamu za Kitanzania

Watazamaji wa filamu za Kitanzania wamekuwa wakishabikia filamu za Kitanzania kutokana na sababu anuwai. Miongoni mwa sababu hizo ni kuwapenda wasanii waliowazoea wakati wakiigiza katika drama za runinga, warembo waliowahi kushinda mashindano ya ulimbwende, wasanii maarufu wa fani nyingine tofauti na maigizo walioamua kuingia kwenye sanaa ya filamu, pamoja na watu maarufu walioamua kucheza filamu. Hii, kwa upande mwingine, yaonesha kuwa kuwapa watazamaji falsafa zitakazoweza kuwabadilisha kwa namna chanya kupitia filamu za Kitanzania wanazozitazama si suala la kipaumbele. Filamu nyingi za Kitanzania zenye U-Nigeria zimekuwa zikitawaliwa na magari makubwa ya kifahari, majumba makubwa ya kifahari, watu waliovaa mavazi ya gharama, waliopambwa na nywele za thamani huku mambo yanayojadiliwa kwenye filamu hizo yakiwa si mambo yanayoweza kupatikana katika jamii wanayoishi. Watazamaji wamekuwa wakivutika na samani wanazoziona na si ujumbe uliofungashwa kwenye filamu wanazozitazama kwa sababu maisha yao na masuala yanayojadiliwa katika filamu yako mbali sana na uhalisi wa maisha yao. Kwa kifupi, maisha ambayo huwa wanayaona kwenye filamu na kuvutika nayo huwaacha watazamaji kwenye ufantasia.

Akishadidia jambo hili, Mwakilama (2013)[5] anasema:

---

[5]John Mwakilama ni mtayarishaji filamu na msomi wa sanaa ya filamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mahojiano yamefanyika kupitia simu ya mkononi Aprili 27, 2013.

> Mimi nalaumu kuwapo filamu za Kitanzania kwa sababu zinaondoa vijana vijijini kuja mjini. Tatizo hazioneshi ukweli. Filamu hizi zimekuwa zikibeba maudhui ya watu wanaotoka vijijini na kuja mjini na kupata maisha mazuri. Zimekuwa hazijengi hoja nzuri kuonesha namna hawa vijana wanavyozipata hizo pesa. Wamekuwa wakionesha vijana wakipata pesa hizo kwa namna rahisi sana. Kwa hivyo, filamu hizi zimekuwa zikiondoa nguvu kazi.

Uigizaji unaotendwa katika filamu za Kitanzania nao umeacha athari kwa watazamaji wa filamu ambao wameanza kuiga namna ya uongeaji wa ki-Nigeria katika mazungumzo yao ya kawaida. Pia, kutokana na maisha ya kibwanyenye yanayooneshwa katika filamu nyingi za Kitanzania, watazamaji wa filamu za Kitanzania nao wameanza kuiga namna ya ujenzi wa majumba makubwa yenye kufuata mtindo wa ki-Nigeria. Pia, mavazi ya ki-Nigeria yamekuwa na athari kwa Watanzania ambao wamekuwa wakiyatumia katika dhifa mbalimbali za kijamii na hivyo kuonekana kama ni mavazi ya kawaida kwa Mtanzania (Kasiga, 2013).

Akizungumzia mtagusano huo, Rwabona[6] (2013) anasema:

> Tunaweza tukajikuta *tunashare culture* (tunakuwa na utamaduni unaofanana) na kufanya utamaduni wetu kutoka Nigeria, hivyo unaweza kukuta siku moja mama anaweza kugombana na baba kisha akaanza kumgombeza kwa namna ya ki-Nigeria−yote hiyo ikiwa ni kutokana na filamu zetu kuiga vitu vingi kutoka Nigeria na hivyo kufanya filamu za Kitanzania kukosa utamaduni na kuzifanya kuwa na utamaduni usio wa Kitanzania na pia usio wa ki-Nigeria.

Mtaalamu huyu wa filamu alikuwa akielezea namna filamu ilivyo na uwezo mkubwa wa kutengeneza utamaduni mpya ndani ya jamii kutokana na athari yake kubwa ya mawasiliano. Kwa hiyo, kutokana na uigaji wa utayarishaji wa filamu za ki-Nigeria katika filamu za Kiswahili nchini Tanzania kumekuwa na hatari ya kupoteza upekee wa utamaduni ambao kupitia filamu za Utanzania ungekuwa ukioneshwa. Kukosekana kwa utamaduni wa Watanzania kupitia filamu zao sambamba na kuwa "doto" wa filamu za ki-Nigeria kunaweza kufanya filamu za Kitanzania kuwa katika njia panda kati ya utamaduni wa ki-Nigeria na matukio ya kubuni yaliyopo katika filamu za ki-Nigeria.

---

[6]Sikalion Rwabona ni mtayarishaji wa filamu, na mhadhiri wa masomo ya filamu kutoka Chuo Kikuu Cha Dodoma.
Mahojiano haya yamefanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Januari 1, 2013.

Msangi (2013)[7] katika kujadili athari za U-Nigeria katika utayarishaji wa filamu za Kitanzania, anasema:

> Athari kubwa ambayo ni nzuri, japo ina kaubaya kake *somewhere* (mahali fulani) ni Watanzania watazamaji wa filamu za ki-Nigeria au zenye mrengo wa ki-Nigeria kuwa *so much exposed* (kuoneshwa sana) kwa utamaduni wa Nigeria. Vithibitisho utaona kwenye harusi zetu wanawake wakiwa na vilemba kama vya akina mama wa ki-Nigeria. Pia, utaona majumba tunayojenga siku hizi ni sawa na yale makasri ya ki-Nigeria. Kwa upande mbaya ni kwamba sasa Watanzania wanaanza kufata uchawi wa ki-Nigeria hadi huko unakotoka.

Hiluka (2013)[8] naye anasema:

> *Nollywood* imeleta athari kubwa ya kiutamaduni nchini na Afrika kwa ujumla kwa kubadilisha baadhi ya tamaduni zetu. Jamii zetu siku hizi zimekuwa na mitazamo inayotokana na utamaduni wa ki-Nigeria na kuifanya tasnia ya filamu nchini kubaki kuwa sekta ya kuganga njaa tu. Wasanii wetu wanadhani kuwa wasipovaa kama wa-Nigeria hawatapendeza, wasipoigiza kama wafanyavyo wa-Nigeria wataonekana hawajui. Matokeo yake tumejikuta tukisimulia hadithi za wa-Nigeria badala ya hadithi zetu.

Masasi (2013)[9], mwigizaji na mwandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania akiongelea kuhusu madhara ya U-Nigeria kwa watazamaji wa filamu za Kitanzania, anasema:

> Filamu zetu zinatangaza utamaduni wa watu wengine. Lengo kubwa la sanaa yoyote ni kutangaza utamaduni wa watu wake. Hivi sasa tunachomiliki kwenye filamu zetu ni lugha tu, ingawa hata yenyewe inapotoshwa kutokana na maneno mengi ya Kiingereza kuingizwa katika filamu hizo. Na hiyo inazifanya kushindwa kuingia katika soko la filamu za kimataifa, kwa sababu hatuna jambo la kulisimamia kupitia filamu zetu.

---

[7]Philemon Msangi ni mtayarishaji wa filamu nchini Tanzania. Mahojiano haya yameyafanyika kupitia mtandao wa facebook Aprili 28, 2013.

[8]Bishop Hiluka ni mwandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili, mjumbe wa Bodi ya Filamu Tanzania na Katibu Mkuu Mstaafu wa Shirikisho la Filamu Tanzania (TAFF). Mahojiano haya yamefanyika kwa simu ya mkononi Aprili 29, 2013.

[9]Bakari Masasi ni mwigizaji wa filamu, mwandishi wa miswada ya filamu na msomi wa fani ya Mawasiliano ya Umma. Mahojiano haya yamefanyika kwa njia ya simu Aprili 29, 2013.

Kwa kumalizia, U-Nigeria uliopo kwenye filamu za Kitanzania umewafanya Watanzania waishi ki-Nigeria katika ardhi ya Watanzania. Filamu hizi zimekuwa mbali na jadi zao, mambo yanayowaweka kwa ukaribu pamoja na asili nyingine muhimu zinazowafanya wawe, yaani asili zenye kuwatambulisha kwa kuwatofautisha miongoni mwa jamii nyingine za kiliumwengu.

### 3.2 Tija za U-Nigeria kwa Watazamaji wa Filamu za Kitanzania

Jamii nyingi za Kiafrika zimekuwa na tamaduni zinazoshabihiana. Hivyo, baadhi ya maudhui yaliyopo katika filamu za ki-Nigeria yamekuwa yakigusa maisha ya kila siku ya Mtanzania. Katika filamu za ki-Nigeria, hasa zile zenye kuzungumzia masuala ya kishirikina zilizokuwa maarufu kwenye miaka ya 2000, maudhui yake yamekuwa yakigusa maisha ya Watanzania. Ushirikina kwa maeneo ya nchini Tanzania umekuwa ni mjadala usiokwisha. Katika maeneo ya Kanda ya Ziwa kumekuwa na rekodi nyingi za mauaji ya vikongwe wenye macho mekundu kwa kudaiwa kuwa ni wachawi (Kasiga, 2013). Pia, watu wenye ulemavu wa ngozi wamekuwa wakiuawa kwa shabaha ya kupata utajiri wa migodini na kwenye shughuli za uvuvi. Mkoa wa Mbeya nao umekuwa na matukio ya kushtua ya uuzaji wa ngozi za binadamu kwa matukio yaliyoripotiwa 1999 na kujirudia tena mwaka 2001. Matukio hayo ya mkoani Mbeya yamekuwa yakienda sambamba na watu kupigwa marungu nyakati za usiku na kusababisha vifo vya watu mbalimbali−yote yakiwa na yanasukumwa na nia ya kishirikina (Kasiga, 2013). Katika mkoa wa Kigoma, watu wenye vipara wanaishi kwa wasiwasi maana vichwa vyao vimekuwa na soko zuri katika nchi jirani. Kwa mantiki hiyo, filamu zenye U-Nigeria zimekuwa zikitoa mafundisho mema kwa Watanzania kuhusu mambo ya kishirikina yenye kurudisha nyuma maendeleo. Kutoa mafunzo hayo kumekuwa kukiambatana na uoneshwaji wa ubaya wa matukio hayo ya ushirikina kwa uhai wa jamii yenye kuthamini utu na haki za binadamu wote.

Licha ya sanaa hii ya filamu za Kitanzania kutawaliwa na U-Nigeria, bado imeweza kuwa sanaa mashuhuri iliyo na uwezo wa kuwafikia watu wa rika tofauti, jinsi tofauti, imani tofauti na jamii tofauti. Uwezo wake wa kuifikia hadhira yake kwa urahisi umewezesha makusudio ya watayarishaji wa filamu kufika kwa watazamaji kwa mafanikio. Filamu za Kiswahili nchini Tanzania zimeweza kufanikisha malengo yake kwa watazamaji tofauti na sanaa nyingine za fasihi zinavyokumbana na changamoto ya kuifikia hadhira yake. Matumizi ya maneno na ishara zinazojengwa kwa kutumia picha jongefu yameifanya sanaa ya filamu za Kitanzania kuweza kuwafikia watazamaji wengi. Uwasilishaji wake wenye kutumia picha jongefu na maneno umerahisisha mawasiliano kwa mtu yeyote mwenye uwezo wa kusikia kuweza kufikiwa na maudhui ya filamu. Sanaa nyingine za fasihi zimekuwa zikitumia njia ya maandishi ambayo imekuwa ikieleweka kwa wale wawezao kusoma.

Kwa mujibu wa udodosi uliofanywa kupitia mitandao mbalimbali yenye kukusanya maoni ya watazamaji wa filamu wa Kitanzania, imedhihirika kuwa utayarishaji wa filamu za Kitanzania unazidi kukua kwa kasi. Mathalani, maoni ya watazamaji kuhusu ubora wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania katika mtandao wa Filamu Central wa Tanzania yalionesha matokeo yafuatayo:

i. Kura 43 sawa na 53% zilionesha kukua kwa utayarishaji wa filamu za Kitanzania;
ii. Kura 22 sawa na 27% zilionesha kuwa ubora wa utayarishaji wa filamu za Kitanzania haujaongezeka; na
iii. Kura 16 sawa na 20% zilionesha kuwa, ubora wa utayarishaji wa filamu za Kitanzania umeshuka.

Katika utafiti huo, idadi ya watazamaji filamu 81 walipiga kura kutoa maoni mtandaoni.[10] Kwa kutazama maoni hayo ya watazamaji wa filamu, tunaona kukua kwa utayarishaji wa filamu za Kitanzania. Hata hivyo, bado jitihada za msingi zinahitajika ili kuzifanya filamu za Kitanzania ziwe karibu na mazingira yake.

Kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya filamu za Kitanzania, serikali ya Tanzania, kupitia Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) imeanza kuhakikisha kuwa sanaa ya filamu nayo inachangia pato la taifa. Hivi sasa mpango huo umeshahusisha usajili wa kazi zote za filamu nchini kabla ya kazi hizo kuwafikia watumiaji. Kupitia mpango huo, hakuna kazi yoyote ya filamu itakayoruhusiwa kuzalishwa au kusambazwa pasipo kusajiliwa na kuwekewa stempu ya kodi kutoka kwenye mamlaka hiyo. Ukusanyaji huo wa kodi unatarajiwa kuwezesha serikali katika ujenzi wa miundombinu ya utayarishaji wa filamu za Kitanzania pamoja na miundombinu mingine ya kimaendeleo. Inaaminika kuwa ikiwa ukusanyaji wa mapato bila ya kuwaumiza watayarishaji wa filamu utatiliwa mkazo, Watanzania watanufaika na filamu zinazotayarishwa nchini mwao.

Kwa upande wa wasanii kupitia uanzishwaji wa mashirikisho ya wasanii hususani Shirikisho la Wasanii wa Filamu Tanzania (TAFF) pamoja na vyama vya wasanii wanaopatikana katika shirikisho hilo, inategemewa kutakuwa na fursa ya kuweza kupeana uzoefu wa fani na hatimaye kuweza kuinyanyua tasnia. Pia, kuzinduliwa kwa mfuko wa uwezeshaji wa wasanii kupitia Wizara ya Habari, Sanaa na Michezo ya Tanzania, kutawawezesha wasanii kukopa na kupata mitaji itakayoweza kuwainua kupitia kiwanda chao cha ubunifu.

## 4.0 Hitimisho

---

[10] Matokeo haya yamechukuliwa Januari, 1, 2016 kutokahttp://filamucentral.co.tz

Tunakazia umuhimu wa kuwapo kwa uimara wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania na utamaduni wake. Filamu, kama hadithi ibebayo vitendo na hisia (drama) zinazotendwa na waigizaji, inapaswa kuwa sehemu ya historia, silika, na maisha ya jamii inamotoka. Kwa kuwa filamu ya Kiswahili nchini Tanzania huchezwa katika mazingira ya jamii ya Watanzania, haina budi kuyawasilisha mazingira hayo na kuwavuta wanajamii wanaopatikana katika mazingira hayo waweze kubadilika kifikra. Tunawanasihi watayarishaji wa filamu za Kiswahili-Tanzania wakumbuke kuwa jamii isiyokuwa na sanaa inayowatambulisha ni jamii inayopoteza uasili wake. Filamu, kama utamaduni mpya wa vijana Watanzania wenye kiu ya kuonesha utamaduni na nafasi yao ya kijamii, inabidi itambue kuwa taifa lenye vijana walioazima utamaduni, au waliokopeshwa utamaduni halina heshima kwenye uso wa dunia.

## Marejeleo

Boggs, J. and D. Petrie (2000). *The Art of Watching Films*. California: Mayfield Publishing Company.

Diang'a, R . (2013).*Analysis of Style and Content in Selected Kenyan Films 1980 to 2009*, Ph.D Thesis, Kenyatta University (Unpublished).

Diawara, M. (1992).*African Cinema: Politics & Culture*.Indiana:Indiana University Press.

Durotoye, A.A. (2003). "Culture, Art and Film in an African Society: An Evaluation." *Nordic Journal of African Studies, 12(1): 49-56.*

Eregare E.A and A.O. Afolabi (2009). "The Effects of Globalization and Deregulation on Nigerian Culture Industries." *Journal of Social Science* ,21(2):145-151.

Hayness, J. (2000). *Nigerian Video Films*. Ohio: Ohio University Center for International Studies.

Hussein, J.W. (2005). "The Functions of African Oral Arts: The Arsi-Oromo Arts in Focus" *African Study Monographs*, 26 (1): 15-58.

Innocent, E. U. (2011)."The Representation of African Traditional Religion and Culture in Nigeria Popular Films."*Politics and Religion,* 5: 1-15

Kasiga, G. (2013).*U-Nigeria katika Filamu za Ki-Tanzania: Chanzo, Sababu na Athari kwa Wa-Tanzania,* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapiswa).

Kasiga, G. (2008)."Tanzania Growing Film Industry and Job Opportunities for Youth,"Makala iliyotolewa kwenye Kongamano la Dunia kuhusu Maendeleo Endelevu, Saskechewan: Chuo Kikuu cha Regina, 13-17 Mei 2008.

Keyan, T. and Maureeen, E. (1995). "Perspectives on Orality in African Cinema."*Oral Tradition,* 10/1: 111-128

Kileo, S. (2011). *Nafasi ya Maudhui ya Filamu za Kiswahili katika Kuakisi Masuala Muhimu ya Kijamii.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Madumulla, J.S. (1993). "Mwandishi wa Riwaya ya Kiswahili na Suala la Ukweli wa Maisha" *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji: Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania* (kur. 141-153). Dar es Salaam: TUKI.

Masimbi, R. (2010) "Kifo cha Utamaduni wa Mtanzania" katika gazeti la *Mwananchi* laMei 7, uk 2.

Mrikaria, S.E. (2007). "Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya," *Swahili Forum* 14: 197-206.

Ruhumbuka, G. (2003). "Tafsiri za Fasihi za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili," *Makala za Semina ya Waandishi wa Kiswahili*, III (kur. 259-271). Dar es Salaam: TUKI.

Thackway, M. (2003) *Africa Shoots Back: Alternative Perspectives Sub-Saharan Francophone African Film*.Indiana: Indiana University Press.